**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

**MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI INATANGAZA NAFASI ZA KAZI KAMA IFUATAVYO.**

**(1). FUNDI MAGARI DARAJA LA III Ngazi ya Mshahara (ZPSF-06) Nafasi moja Unguja**

***Sifa za Muombaji.***

- Awe ni Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 45
- Awe amehitimu cheti kutoka katika Chuo kinachotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Ordinary Diploma in Auto Mechanics Engineering
- Ordinary Diploma in Mechanical Engineering
- Ordinary Diploma in Automative Engineering

**MAJUKUMU YA KAZI:**

1. Kusaidia kukarabati magari na vifaa vyote vya karakana.
2. Kutunza vifaa vyote vilivyomo ndani ya karakana.
3. Kuhakikisha usalama wa karakana.

**(2) DEREVA DARAJA LA III Ngazi ya Mshahara (ZPSE-03) Nafasi Moja Pemba.**

***Sifa za Muombaji.***

- Awe ni Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 45
- Awe amehitimu Cheti kutoka katika Chuo kinachotambulikana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Cheti kutoka Chuo Cha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali LEVEL III katika Fani ya Umeme wa Magari
- Cheti cha Kidato cha nne
- Leseni ya Udereva Class A, B1 na D.

**MAJUKUMU YA KAZI:**

1. Kukagua gari aliyopangiwa kazi kabla ya kutumika kila siku.
2. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote.
3. Kutoa taarifa kwa tatizo lolote litakalojitokeza juu ya chombo husika.
4. Kujaza (Log book) kabla ya kufanya safari aliyopangiwa.
5. Kutoa taarifa kwa Mkuu wake wa kazi juu ya haja ya kufanyiwa Mtengenezo gari baada yakumjuulisha tatizo.
6. Kuwa tayari kufanya safari yoyote ya kazi na kwa wakati atakaopangiwa na Mkuu wake wa kazi.
7. Kuwa na kumbukumbu ya wakati wa gari inapohitaji kupelekwa karakana kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo.
8. Kuegesha gari wakati inapomaliza shughuli zake za siku ndani ya eneo la taasisi na kuikabidhi kwa Walinzi wa zamu.
9. Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

**(3) MWALIMU WA UJASIRIAMALI DARAJA LA II Nafasi 1Unguja ngazi ya Mshahara (ZPSH-08)**

***Sifa za Muombaji***

- Awe ni Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 45
- Awe amehitimu Shahada ya kwanza ya Ujasiriamali kutoka katika Chuo kinachotambulikana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Bachelor of Business Administration and Entrepreneurship Development
- Bachelor of Science in Economics
- Bachelor of Arts in Business Economic
- Bachelor Of Arts in Economics
- Bachelor of Management of Social Development
- Bachelor of Marketing and Entrepreneurship
- Bachelor of Entrepreneurship and Innovation Management

**MAJUKUMU YA KAZI:**

1. Kufundisha katika Ngazi ya Cheti.

2. Kutayarisha mpangilio wa masomo wanayofundisha (Scheme of Work) kila mwisho wa mwaka au inapohitajika.
3. Kutayarisha na kusimamia mafunzo ya muda mfupi na semina mbali mbali pale inapohitajika.
4. Kutafuta na kubuni mbinu mbali mbali za kukuza na kuendeleza elimukatika fani na vyuo husika.
5. Kushiriki kazi za vitendo za darasani (Teaching Practice).
6. Kufany kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

**(4) AFISA SHERIA DARAJA LA II NAFASI 1 Ngazi ya Mshahara (ZPSH-06)**

***Sifa za Muombaji***

- Awe ni Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 45
- Awe amehitimu Shahada ya kwanza ya Sheria katika Chuo kinachotambulikana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Bachelor of Law and Sharia
- Bachelor of Laws (llb)
- Bachelor of Arts and Bachelor of Laws
- Kuhusu sheria kwa muombaji wa Fani ya Sheria aliehitimu kuanzia 2019 na kuendelea atalazimika kuwasilisha Cheti cha kuhitimu mafunzo ya Vitendo kutoka Skuli ya Sheria.
- Kwa muombaji amehitimu mafunzo yake kabla ya 2019 sio lazima kuwasilisha Cheti cha Mafunzo ya Vitendo.
- Wahitimu waliosoma Skuli ya Sheria ya Tanzania au Skuli za Sheria za Nje ya nchi itawalazimu kuwasilisha uthibitisho wa vyeti vyao kuhitimu skuli ya mafunzo ya sheria ya Zanzibar.

**MAJUKUMU YA KAZI:**

1. Kushiriki katika kutafsiri Sheria, Kanuni na hati nyengine za Kisheria.
2. Kusaidia kutoa huduma za kisheria kila inapohitajika.
3. Kushiriki katika kufatilia utekelezaji wa Kanuni na Sheria zinazohusiana na kazi za Mamlaka.
4. Kushiriki kuandika na kupitia mikataba, kodi na utoaji wa leseni katika sekta zinazodhibitiwa.
5. Kushiriki katika kupitia rufaa, taratibu na ufuatiliaji wake kisheria.
6. Kushiriki katika kutoa michango katika tafiti za kisheria na musuala mengine ya kisheria ambayo zinazohusiana na Sekta zinazodhibitiwa kulingana na kazi za Mamlaka.
7. Kushiriki katika Kuratibu michango na ushauri wa kisheria na kuhusiana na malalamiko yam toa na mpokeaji huduma.
8. Kusaidia kuhifadhi kumbukumbu za majadala ya kesi zinazohusiana na Mamlaka.
9. Kufanyakazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

**(5) MWALIMU WA ELECTRONICS DARAJA LA II (ZPSH-08) Nafasi moja Unguja**

***Sifa za Muombaji.***

- Awe ni Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 45
- Awe amehitimu Shahada ya Electronics kutoka katika Chuo kinachotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Shahada ya Telecommunications na Electronics Engineering
- Bachelor of Electronics and Electrical Engineering
- Bachelor of Electronic and Communication Engineering

**MAJUKUMU YA KAZI:**

1. Kufundisha katika ngazi ya Cheti
2. Kutayarisha mpangilio wa masomo wanayofundisha (Scheme of Work) kila mwisho wa mwaka au inapohitajika.
3. Kutayarisha na kusimamia mafunzo ya muda mfupi na semina mbali mbali pale inapohitajika.
4. Kutafuta na kubuni mbinu mbali mbali za kukuza na kuendeleza elimu katika fani na vyuo husika.
5. Kushiriki kazi za vitendo darasani (Teaching Practice).
6. kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

**(6) Mwalimu wa Ukalimani nafasi moja Unguja ngazi ya Mshahara (ZPSF-06).**

***Sifa za Muombaji.***

- Awe ni Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 45
- Awe amehitimu Stashahada ya lugha za Alama kutoka katika Chuo kinachotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na Elimu ya Stash-hada ya Elimu Mjumuisho na Mahitaji Maalum.

**MAJUKUMU YA KAZI:**

- Kutoa taaluma ya ukalimani kutoka lugha ya mazungumzo kwenda katika lugha ya alama
- Kufundisha ngazi ya cheti
- Kutunga na kusahihisha mitihani na kuwasilisha kunakohusika
- Kufundisha nadharia na mbinu za ukalimani
- Kuwaandaa wanafunzi kwa kazi halisi
- Kufanya ya tathmini ya wanafunzi na kutoa mrejesho
- Kufanya kazinyengine kulingana na majukumu yako kama utakavyopangiwa na mkuu wako wa kazi

JINSI YA KUOMBA

Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya kielectronik kwenye Mfumo wa maombi ya Ajira (Zan-Ajira) kupitia anuani ifuatayo: http://portal.zanajira.go.tz Kuanzia 10/09/2025 Hadi Tarehe 16/09/2025. saa Tisa na nusu.

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali www.zvta.go.tz.

Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa Zan Ajira (kwa njia ya kielectroniki pekee):-

MKURUGENZI MTENDAJI
MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI
SLP 4805,
ZANZIBAR.

- Muombaji anatakiwa kuanisha nafasi ya kazi anayoiomba
- Muombaji atakaewasilisha Progressive Report au Statement of Results pekee maombi hayatazingatiwa.
- Kwa waombaji waliosoma Vyuo vya nje ya Tanzania wanatakiwa wawasilishe nakla ya Cheti cha uhakiki kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).
- Kwa msaada wa Kitaalamu wasiliana na 0774056160/0777147335

AHSANTENI.